ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

# FIDIA eNEWSLETTER

TOLEO LA TISA | OKTOBA-DESEMBA 2025 | www.wcf.go.tz

## WCF yapongezwa kwa utoaji huduma bora kwa wananchi



Karibu Sana

Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

# YALIYOMO


- WCF yapongezwa kwa utoaji huduma bora kwa wananchi
- Madaktari 150 wapatiwa mafunzo ya kuboresha huduma kwa wanufaika wa WCF
- WCF yawajengea uwezo makatibu wa kamati za bunge kuhusu masuala ya fidia kwa wafanyakazi
- WCF yaungana na jamii kukuza ujumuishi wa watu wenye ulemavu


Jarida Mtandaoni
Skanii Kodi ya QR
Hapo Chini


TIMU YA WAHARIRI

MWENYEKITI
Dkt. John K. Mduma

MHARIRI MKUU
Laura G. Kunenge

MHARIRI MSAIDIZI
Sophia F. Mtakasimba

WACHANGIAJI
Mcharo S. Mrutu
Meseka Z. Kadala
Lilian R. Shembilu



# Dibaji

## Neno Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu

**Ninapenda** kuchukua fursa hii kuwakaribisha wadau wetu wote katika Jarida la Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) la Robo ya Pili ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, linalohusisha kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025.

Robo hii imekuwa ya mafanikio makubwa kwa Mfuko, ambapo tumeendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa wanufaika wetu kwa kuzingatia misingi ya uwazi, ufanisi na uwajibikaji. Katika kipindi hiki, Mfuko umeendelea kuboresha mifumo ya utoaji wa fidia, kuimarisha usimamizi wa madai yatokanayo na ajali na magonjwa ya kazini, pamoja na kuongeza juhudi za elimu na uhamasishaji kwa waajiri na wafanyakazi kote nchini kuhusu wajibu na haki zao chini ya Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

Aidha, tumeendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wetu wakuu wakiwemo waajiri wa sekta ya umma na binafsi, vyama vya wafanyakazi, taasisi za serikali na binafsi, pamoja na wataalamu wa afya, ili kuhakikisha huduma za fidia zinawafikia walengwa kwa wakati na kwa viwango vinavyokubalika. Ushirikiano huu umeendelea kuwa nguzo muhimu katika kutekeleza dhamira ya Mfuko ya kulinda ustawi na usalama wa wafanyakazi nchini.

Tunapofunga mwaka 2025 na kuukaribisha Mwaka Mpya 2026, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote wa WCF kwa ushirikiano, uaminifu na mchango wao mkubwa katika kufanikisha majukumu ya Mfuko. Mafanikio tuliyoyapata yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na mshikamano wenu na imani mliyoendelea kuionesha kwa taasisi yetu.

Kwa niaba ya Bodi ya Wadhamini, Menejimenti na wafanyakazi wote wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, napenda kuwatakia wadau wetu wote Heri ya Mwaka Mpya 2026. Tunawatakia afya njema, mafanikio na mwaka uliojaa tija katika majukumu yenu binafsi na ya kitaasisi. WCF itaendelea kuwa mshirika wenu wa karibu katika kulinda haki, usalama na ustawi wa wafanyakazi kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Asanteni kwa kuendelea kushirikiana nasi

**Dkt. John K. Mduma**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano Mhe. Deus Sangu akizungumza na Menejimenti ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Jijini Dodoma wakati wa ziara yake katika Ofisi za Makao Makuu ya WCF.*

# WCF YAPONGEZWA KWA UTOAJI HUDUMA BORA KWA WANANCHI

**Na Mwandishi Wetu**

**Waziri** wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano Mhe. Deus Sangu ameupongeza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa hatua kubwa ilizochukua katika kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wananchi, hususan utoaji wa fidia kwa wafanyakazi wanaokumbana na madhila ya ajali ama ugonjwa unaotokana na kazi.

Mhe. Waziri alitoa pongezi hizo Desemba 10, 2025 Jijini Dodoma wakati wa ziara yake katika Ofisi za Makao Makuu ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) alipokutana na Menejimenti na baadhi ya watumishi wa WCF kwa lengo la kujua majukumu ya Mfuko huo sambamba na kutoa maelekezo ya kiutendaji yanayolenga kuongeza tija na ufanisi kuendana na maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania.

"Huduma hizo bora zimechangia kuimarisha imani ya wananchi kwa Mfuko, wafanyakazi wanaopatwa na majanga kutokana na kazi wamekuwa wakipatiwa huduma kwa wakati na kwa kiwango kinachostahili, jambo ambalo limeongeza ufanisi na kupunguza usumbufu kwa wafanyakazi." Alisema Mhe. Sangu

Katika hatua nyingine, Waziri Sangu aliitaka Menejimenti ya WCF kuendeleza ubunifu katika utekelezaji wa majukumu yao, ikiwemo kuongeza nguvu ya mifumo mipya ya kidijitali inayoboresha mbinu za utoaji huduma kwa wakati na ufanisi na kufikia wananchi kwa haraka zaidi.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Rahma Kisuo, aliihamasisha Menejimenti ya Mfuko huo kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu majukumu na huduma zinazotolewa na WCF, ili kuongeza uelewa na ushiriki wa waajiri wengi zaidi.



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Rahma Kisuo akizungumza wakati wa ziara hiyo.*

**Inaendelea...**

**Kutoka Ukurasa wa 01**

"Elimu kwa umma ni nguzo muhimu katika kuhakikisha waajiri wanaelewa wajibu wao na kunufaika ipasavyo na huduma za WCF," alisema Mhe. Kisuo.

Akizungumza kwa niaba ya Menejimenti ya WCF, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Dkt. John Mduma, alisema WCF imejipanga kuendelea kuboresha mifumo ya utoaji huduma kwa lengo la kuhakikisha madai ya fidia yanashughulikiwa kwa wakati, kwa uwazi na kwa ufanisi zaidi.

"Tumejizatiti kuendelea kuboresha mifumo na taratibu zetu ili kila dai la fidia lishughulikiwe kwa haraka na kwa haki, kwa maslahi mapana ya wafanyakazi na waajiri," alisema Dkt. Mduma.




*Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya WCF wakimsikiliza Mh. Waziri Sangu*

Ziara hiyo imeonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha taasisi zake ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi, huku WCF ikiendelea kujipambanua kama chombo muhimu katika ulinzi na ustawi wa wafanyakazi nchini.

# WCF YAENDELEA KUWAJENGEA UWEZO MAAFISA RASILIMALI WATU NA MAAFISA USALAMA KAZINI

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Rasilimali Watu na Maafisa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kutoka mikoa ya kanda ya Pwani na Kusini, lengo likiwa ni kuongeza uelewa kuhusu masuala ya fidia pamoja na usalama na afya kazini. Mafunzo hayo yamefanyika mjini Mtwara kuanzia tarehe 11 hadi 12 Novemba 2025.




*Watoa mada wakati wa mafunzo kwa maafisa rasilimali watu na usalama kazini*

Akifungua rasmi mafunzo hayo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini, Dkt. Abdulsalaam Omar, alisema mafunzo hayo ni muhimu katika kuhakikisha waajiri na wafanyakazi wanapata elimu sahihi kuhusu haki zao za fidia na namna bora ya kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi. Alisisitiza kuwa kupitia mafunzo hayo, washiriki wataweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi katika kulinda usalama na afya ya wafanyakazi mahali pa kazi.

Dkt. Omar alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kusimamia dhamira ya kujenga uchumi endelevu na shindani unaolenga kuwawezesha Watanzania kuondokana na umaskini kupitia fursa mbalimbali za uwekezaji. Alibainisha kuwa mafanikio ya dhamira hiyo yanategemea uwepo wa wafanyakazi wenye uhakika wa usalama na afya kazini, na kwamba endapo watapata madhara, ni muhimu wapatiwe fidia stahiki na kwa wakati.

**Inaendelea...**

Kutoka Ukurasa wa 02



*Meneja Tathmini Vihatarishi mahala pa Kazi Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Bi Naanjela Msangi akiwasilisha mada wakati wa mafunzo hayo*

Aidha, Dkt. Omar aliongeza kuwa WCF itaendelea kutoa mafunzo kama hayo katika mikoa mbalimbali nchini ili kuwajengea wadau uwezo wa kubaini na kudhibiti viashiria vya hatari kazini, sambamba na kuongeza uelewa kuhusu taratibu za kuwasilisha madai kwa kutumia mifumo ya kidijitali. Alisisitiza kuwa Mfuko utaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wote wa sekta ya ajira ili kuhakikisha dhamira ya kulipa fidia stahiki kwa wakati inatimia.

Kwa upande wake, Afisa Kazi Mfawidhi wa Mkoa wa Mtwara, Bw. Paskali Kapinga, alisisitiza umuhimu wa washiriki kutumia kikamilifu fursa hiyo adhimu kwa kuuliza maswali na kuchangia hoja mbalimbali, akibainisha kuwa ushiriki wao wa karibu ndiyo njia bora ya kuhakikisha wanapata uelewa wa kina na ufafanuzi wa kutosha kuhusu masuala yote muhimu yanayohusu fidia kwa wafanyakazi.

Naye mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Bi. Iki Omary kutoka SACCOS ya Walimu Newala, alisema mafunzo hayo yamekuwa na manufaa makubwa kwake kwa kuwa yamemjengea uelewa kuhusu masuala ya usalama kazini pamoja na haki na wajibu wa wafanyakazi katika kunufaika na mafao ya WCF endapo watapata ajali kazini
.

Katika mafunzo hayo, mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwemo huduma zinazotolewa na WCF, hatua sahihi za kuwasilisha madai ya fidia, pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijitali ya Mfuko huo ikiwemo WCF Online Portal na WCF Mkononi App, ikiwa ni sehemu ya jitihada za Mfuko kuboresha utoaji wa huduma kwa waajiri na wafanyakazi nchini.



*Baadhi ya washiriki wakifuatilia mafunzo*



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano, Mheshimiwa Rahma Kisuo akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo maalum ya tathmini za magonjwa yatokanayo na kazi kwa madaktari Jijini Tanga.

# MADAKTARI 150 WAPATIWA MAFUNZO YA KUBORESHA HUDUMA KWA WANUFAIKA WA WCF

**Na Mwandishi Wetu**

Jumla ya madaktari 150 kutoka mikoa Saba nchini wamepatiwa mafunzo maalum ya tathmini za magonjwa yatokanayo na kazi, yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa wanufaika wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Mafunzo hayo yaliyofanyika Jijini Tanga, yalifunguliwa na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano, Mheshimiwa Rahma Kisuo, ambaye alisema Serikali inaendelea kuwekeza katika mafunzo ya rasilimali watu ili kuhakikisha wafanyakazi wanaopata ajali au magonjwa yatokanayo na kazi wanapata fidia stahiki kwa wakati na kwa viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Kisuo alisema hadi sasa jumla ya madaktari 1,894 kutoka hospitali na vituo vya afya mbalimbali nchini wameshapatiwa mafunzo ya tathmini za ulemavu unaotokana na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi, huku madaktari wengine 217 wakipatiwa mafunzo ya vitendo (hands-on impairment assessment training).

"Mafunzo haya yanawajengea madaktari wetu uelewa mpana wa taratibu za kuwahudumia wanufaika wa WCF na kuwawezesha kufanya tathmini sahihi ya athari za kibaiolojia zitokanazo na ajali za kikazi au magonjwa yatokanayo na kazi, hatua itakayochochea ufanisi na haki katika ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi." Ameeleza Mhe. Kisuo.

Awali akizungumza, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alisema mafunzo hayo yameandaliwa na Mfuko huo kama sehemu ya jitihada za kuboresha utoaji wa huduma za matibabu na kuhakikisha tathmini za ulemavu zinafanyika kwa usahihi na kwa wakati.

"WCF imeandaa mafunzo haya kama sehemu ya mkakati wake wa makusudi wa kuboresha utoaji wa huduma za matibabu, kwa kuhakikisha tathmini za ulemavu zinafanyika kwa usahihi na kwa wakati, ili kulinda haki na ustawi wa wafanyakazi," aliongeza Dkt. Mduma.



Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo maalum ya tathmini za magonjwa yatokanayo na kazi kwa madaktari Jijini Tanga.

**Inaendelea...**

Kutoka Ukurasa wa 04

Kwa upande wake, mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Dkt. Salma Nassor, amesema mafunzo hayo yameongeza ushirikiano miongoni mwa madaktari na kutoa fursa ya kubadilishana uzoefu kwa lengo la kuboresha huduma kwa wanufaika wa WCF.

"Mafunzo haya yameimarisha ushirikiano miongoni mwetu na kutupa fursa muhimu ya kubadilishana uzoefu, jambo litakalosaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma tunazotoa kwa wanufaika wa Mfuko." Amesema Dkt. Salma Nassor.

Katika mafunzo hayo madaktari kutoka hospitali za umma na binafsi walikutanishwa, kuanzia ngazi ya vituo vya afya hadi hospitali za rufaa, kutoka mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.






# WCF YAUNGANA NA JAMII KUKUZA UJUMUISHI WA WATU WENYE ULEMAVU -MOROGORO

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeungana na makundi ya watu wenye ulemavu nchini katika Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu yaliyoadhimishwa tarehe 3 Desemba, 2025, mjini Morogoro, kwa kushiriki maonesho ya kijamii yaliyoandaliwa sambamba na kilele cha maadhimisho hayo.

Maonesho hayo yaliyoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) yalilenga kuonesha mchango wa taasisi mbalimbali katika kujenga jamii jumuishi, huku WCF ikitumia jukwaa hilo kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zake, hususan matumizi ya mifumo ya kidijitali pamoja na fursa za kiuchumi na kijamii zinazolenga kuwawezesha watu wenye ulemavu.

Akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho hayo, Mgeni Rasmi ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Adam Kigoma Malima, alisema kuwa taasisi za umma zinapaswa kuendelea kubuni mifumo rafiki na jumuishi itakayowezesha watu wenye ulemavu kupata huduma kwa urahisi na kwa usawa.

"Tunapaswa kuondoa vikwazo vyote vinavyowakwamisha watu wenye ulemavu, ili wajione kuwa ni sehemu kamili ya jamii na maendeleo ya nchi," alisisitiza Mhe. Malima.

Kwa upande wake, mmoja wa washiriki wa maonesho hayo ambaye ni mwanachama wa SHIVYAWATA, alisema uwepo wa WCF katika maadhimisho hayo umeongeza uelewa kuhusu haki na fursa zilizopo kwa watu wenye ulemavu.
"Kupitia banda la WCF tumepata elimu muhimu kuhusu huduma za fidia na matumizi ya mifumo ya kidijitali, jambo linalotupa matumaini mapya ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi," alisema mshiriki huyo.

Naye mwakilishi wa WCF Mkoa wa Morogoro ndugu Themistocles Rumboyo aliainisha kuwa Mfuko utaendelea kushirikiana na Serikali na wadau wengine katika kubuni na kuboresha programu zinazolenga kuwafikia watu wenye ulemavu kwa ufanisi zaidi.

"WCF itaendelea kusogeza huduma karibu na jamii na kuhakikisha hakuna mtu anayebaki nyuma, hususan watu wenye ulemavu," alisema ndugu Rumboyo.

Maadhimisho ya mwaka huu yaliendeshwa chini ya kauli mbiu isemayo "Kuendeleza Jamii Jumuishi kwa Watu Wenye Ulemavu kwa Mustakabali na Ustawi wa Jamii", kauli mbiu inayosisitiza umuhimu wa mshikamano wa jamii na taasisi katika kujenga taifa lenye usawa, haki na fursa kwa wote.

**Inaendelea...**



MFUKO WA FIDIA
KWA
WAFANYAKAZI
WCF
Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED
ISO 9001 : 2015


WCF Mkononi App
Available on Playstore and
Appstore. Download Now




Employee Login
Login
Create Account
Get Started


WCF
Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED



# WCF YAWAJENGEA UWEZO MAKATIBU WA KAMATI ZA BUNGE KUHUSU MASUALA YA FIDIA KWA WAFANYAKAZI

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeendesha semina maalum kwa Makatibu wa Kamati za Bunge mjini Morogoro mwezi Novemba 2025, ikilenga kuongeza uelewa wao kuhusu sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, usajili wa waajiri, uwasilishaji wa michango, pamoja na taratibu za uwasilishaji na tathmini ya madai ya fidia kwa wafanyakazi.

Akifungua semina hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya mkakati wa Mfuko wa kuhakikisha watendaji muhimu wa Serikali wanakuwa na uelewa wa kina kuhusu masuala ya fidia, usalama kazini na wajibu wa waajiri.

“Mafunzo haya yamelenga kuwajengea uwezo watendaji wa Bunge ili wawe na uelewa mpana wa mchakato mzima wa fidia kwa wafanyakazi na hivyo kuchangia ufanisi katika usimamizi wa masuala ya ajali kazini na magonjwa yatokanayo na kazi,” alisema Dkt. Mduma.

.Aliongeza kuwa uwekezaji katika uelewa wa watendaji hao ni hatua muhimu katika kuimarisha mifumo ya ulinzi wa wafanyakazi nchini.

“Tunaamini kuwa kuwajengea uwelewa watendaji wa Bunge kutaimarisha zaidi ufanisi katika kusimamia masuala ya ajali kazini, ugonjwa unaotokana na kazi pamoja na utoaji wa fidia kwa wafanyakazi,” alisisitiza.




*Meneja Madai Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Bi. Rehema Kabongo akiwasilisha mada wakati wa semina ya kuwajengea uelewa Makatibu wa Bunge kuhusu Fidia kwa Wafanyakazi.*

Katika semina hiyo, washiriki waliwasilishiwa mada mbalimbali zikiwemo matumizi ya mifumo ya kidijitali ya WCF, huku wakifafanuliwa namna inavyorahisisha utoaji wa huduma kwa waajiri na wafanyakazi. Wataalamu wa Mfuko walieleza kwa kina matumizi ya WCF Portal na WCF Mkononi App, mifumo inayowawezesha wadau kuwasilisha michango, madai ya fidia, kufuatilia hatua za uchakataji pamoja na kupata taarifa kwa haraka.




*Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Adv. Abraham Siyovelwa akiwasilisha mada wakati wa semina ya kuwajengea uelewa Makatibu wa Bunge kuhusu Sheria ya Fidia.*

“Mifumo ya kidijitali imepunguza kwa kiasi kikubwa muda na gharama, huku ikiongeza uwazi na ufanisi katika utoaji wa huduma,” alieleza mmoja wa wawezeshaji wa mafunzo hayo.

Aidha, washiriki walipata ufafanuzi kuhusu mfumo wa e-mrejesho unaowawezesha wafanyakazi kuwasilisha maoni, maulizo na malalamiko yao kwa urahisi zaidi, hatua inayochangia kuboresha uwajibikaji na mawasiliano kati ya Mfuko na wanufaika wake.


Akizungumza kwa niaba ya washiriki, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge, Bw. Michael Chikokoto, aliishukuru WCF kwa kuandaa semina hiyo yenye tija, akibainisha kuwa imeongeza kwa kiasi kikubwa uelewa wao kuhusu majukumu ya Mfuko na mifumo inayotumika.

“Mafunzo haya yametupa uelewa mpana kuhusu sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, majukumu ya WCF pamoja na matumizi ya mifumo ya kisasa katika kushughulikia madai ya fidia,” alisema Bw. Chikokoto.

**Inaendelea...**

## Picha Mbalimbali wakati wa kikao kazi cha makatibu wa bunge na Wafanyakazi wa WCF


























Kutoka Ukurasa wa 07



*Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Dkt. Abdulsalaam Omar akiwasilisha mada wakati wa semina ya kuwajengea uelewa Makatibu wa Bunge kuhusu Masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi.*

Semina hiyo imeonesha dhamira ya WCF ya kuendelea kushirikiana na taasisi za Serikali katika kujenga uwezo wa wadau wake, hatua inayolenga kuimarisha ufanisi, uwazi na haki katika utoaji wa fidia kwa wafanyakazi wanaopatwa na madhila yatokanayo na kazi hapa nchini.

## TANGAZO



# HAPPY CORNER



# HABARI KATIKA PICHA


















Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

Jarida hili limeandaliwa na
Kitengo cha Uhusiano kwa Umma:
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,
S.L.P 329, 41104 Dodoma,
TANZANIA